



## TAARIFA KWA UMMA

### KUKAMILIKA KWA AWAMU YA NNE YA UDAHILI WA SHAHADA YA KWANZA KATIKA TAASISI ZA ELIMU YA JUU NCHINI KWA MWAKA WA MASOMO 2021/2022

Dar es Salaam, Tarehe 23 Oktoba, 2021

#### 1.0 UTANGULIZI

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) inapenda kufahamisha umma na wadau wa Elimu ya Juu nchini kuwa Awamu ya Nne na ya mwisho ya Udahili kwa ngazi ya Shahada ya Kwanza katika Taasisi za Elimu ya Juu nchini kwa mwaka wa masomo 2021/2022 umekamilika. Majina ya waombaji waliodahiliwa katika Awamu ya Nne yanatangazwa na vyuo husika.

#### 2.0 WAOMBAJI WALIODAHILIWA KATIKA CHUO ZAIDI YA KIMOJA

Waombaji waliodahiliwa katika chuo zaidi ya kimoja katika Awamu ya Nne na wale ambao hawakuweza kuthibitisha udahili katika awamu zilizopita wanasisitizwa ***kuthibitisha udahili wao katika chuo kimojawapo kuanzia tarehe 24 Oktoba hadi 6 Novemba, 2021*** kwa kutumia namba maalum ya siri iliyotumwa kwa ujumbe mfupi kupitia namba zao za simu au barua pepe walizotumia wakati wa kuomba udahili. Wale ambao hawatapata kwa wakati ujumbe huo, wanashauriwa kuingia kwenye mifumo ya udahili ya vyuo walivyodahiliwa na kuomba kutumiwa ujumbe mfupi wenye namba maalum ya siri ili kuweza kujithibitisha katika chuo husika. Aidha, uthibitisho wa udahili ufanyike kupitia akaunti ambayo muombaji alitumia wakati wa kuomba udahili.

Orodha ya majina ya waombaji waliodahiliwa katika chuo zaidi ya kimoja katika Awamu ya Nne na wale ambao walishindwa kuthibitisha udahili katika awamu zilizopita imewekwa katika tovuti ya TCU ([www.tcu.go.tz](http://www.tcu.go.tz)).

### **3.0 WITO KWA WAOMBAJI UDAHILI**

Waombaji udahili wa Shahada ya Kwanza wanakumbushwa kuwa masuala yote yanayohusu udahili au kujithibitisha katika chuo kimoja yawasilishwe moja kwa moja kwenye vyuo husika.

Imetolewa na:



Dkt. Telemu J. Kassile  
**Kny: KATIBU MTENDAJI**  
**TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA**